JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS**

**TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

# MWONGOZO WA MASHAURI YA NIDHAMU, RUFAA NA MALALAMIKO KATIKA UTUMISHI WA UMMA

**Umeandaliwa chini ya Kifungu cha 20 cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 [Marejeo ya Mwaka 2019]**

**Toleo la 3 la Mwaka 2024**

KIMEPIGWACHAPA NA MPIGACHA MKUU WA SERIKALI, DODOMA-TANZANIA

**Umeandaliwa na:**
**Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma, S.L.P. 1074, DODOMA.**
**Barua pepe: secretary@psc.go.tz**
**Tovuti: www.psc.go.tz**

# MWONGOZO WA MASHAURI YA NIDHAMU, RUFAA NA MALALAMIKO KATIKA UTUMISHI WA UMMA

## YALIYOMO

DIBAJI ........................................................................ iv

FASILI YA MANENO MBALIMBALI YALIYOTUMIKA............ v

1.0 UTANGULIZI ........................................................ 1

1.1 Madhumuni ........................................................ 1

1.2 Watekelezaji wa Mwongozo .................................. 2

SURA YA PILI ........................................................ 3

2.0 Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa Umma ............ 3

2.1 Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa Umma ............ 3

2.2 Mamlaka nyingine za Nidhamu (Other Delegates) ........... 5

2.3 Makosa ya kinidhamu na adhabu zake ........................ 5

2.3.1 Utoaji wa Adhabu ................................................ 7

2.3.2 Masuala ya Nidhamu na Makosa ya Jinai .................... 7

2.4 Majukumu na Maelekezo ya Utekelezaji ...................... 9

SURA YA TATU ........................................................ 10

3.0 RUFAA KATIKA UTUMISHI WA UMMA ........................ 10

3.1 Mamlaka za Rufaa katika Utumishi wa Umma ................10

3.2 Taratibu za Utekelezaji wa Majukumu ya Mamlaka ya Rufaa ................................................................11

3.2.1 Utaratibu wa jumla wa kuzingatia ..............................11

3.2.2 Kuwasiliana na Mamlaka ya Nidhamu au Rufaa.......... 12

3.2.3 Kumfahamisha Mrufani na Mamlaka ya Nidhamukuhusu uamuzi wa Rufaa. ................................................. 12

3.3 Majukumu na maelekezo ya utekelezaji ....................... 12

SURA YA NNE.......................................................... 13

4.0 MALALAMIKO KATIKA UTUMISHI WA UMMA .............. 13
4.1 Utaratibu wa kuwasilisha malalamiko .............................. 13
4.1.1 Mwajiri .............................................................................. 13
4.1.2 Bodi za Taasisi ........................................................... 13
4.1.3 Katibu Mkuu wa Wizara husika ................................... 13
4.1.4 Katibu Mkuu - UTUMISHI ............................................. 14
4.1.5 Tume ya Utumishi wa Umma....................................... 14
4.1.6 Katibu Mkuu Kiongozi .................................................. 14
4.2 Mambo ya Kuzingatia katika Ushughulikiaji wa Mlalalamiko katika Utumishi wa Umma: ........................ 14
4.2.1 Muda wa kuwasilisha malalamiko................................ 14
4.2.2 Uthibitisho wa malalamiko ........................................... 15
4.2.3 Muda wa kushughulikia malalamiko............................. 15
4.2.4 Kuhitimishwa kwa Malalamiko na Utoaji waUamuzi15
5.0 Tangazo la Mgongano wa Maslahi .................................. 15
6.0 HITIMISHO ............................................................................ 16
7.0 Tarehe ya kuanza kutumika............................................. 16
MFANO WA HATI YA MASHTAKA NA NOTISI.................... 17

## DIBAJI

Mwongozo wa Mashauri ya Nidhamu, Rufaa na Malalamiko unatoa maelekezo mahsusi kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira, Mamlaka za Nidhamu, Mamlaka za Rufaa na Watumishi wa Umma ili kuwajengea uelewa wa pamoja na kuweka utaratibu unaopaswa kuzingatiwa wakati wa kushughulikia mashauri ya nidhamu, rufaa na malalamiko ya watumishi wa Umma.

Mwongozo huu utawasaidia Waajiri, Mamlaka za Ajira, Mamlaka za Nidhamu, Mamlaka za Rufaa, Wanasheria, Maafisa Utumishi na Utawala na Watumishi wa Umma kupata uelewa wa pamoja wa masuala ya msingi na hatua muhimu za kuzingatia wakati wa kushughulikia mashauri ya nidhamu, rufaa na malalamiko. Ni matarajio ya Tume kwamba wadau wote watazingatia Mwongozo huu ipasavyo ili haki iweze, si tu kutendeka bali kuonekana imetendeka.

Ukiukwaji wa Mwongozo huu katika kushughulikia mashauri ya nidhamu, rufaa na malalamiko ya Watumishi wa Umma utachukuliwa kuwa ni kosa la kinidhamu na mhusika atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria.



**Mathew M. Kirama**
**KATIBU**

**TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

## FASILI YA MANENO MBALIMBALI YALIYOTUMIKA

Katika Mwongozo huu, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo;

"Bodi ya Ajira" maana yake ni Chombo katika Taasisi au Mashirika ya Umma ambacho kinateuliwa na Mamlaka ya Ajira kwa ajili ya kusimamia masuala ya ajira katika Taasisi au Shirika husika.

"Kamati" maana yake ni Kamati ya Uchunguzi wa shauri la nidhamu la mtumishi wa Umma.

"kosa la nidhamu" maana yake ni kutenda au kutotenda jambo, kushindwa kuchukua hatua stahiki, kushindwa kufikia malengo yaliyowekwa au kutotekeleza majukumu ipasavyo ambako kutasababisha mtumishi wa Umma achukuliwe hatua za kinidhamu chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma ikiwemo; kukiuka Kanuni za Maadili na Mwenendo kwa Watumishi wa Umma, Maadili ya Taaluma na Maadili ya Viongozi wa Umma au kosa lolote lililoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Kanuni za Utumishi wa Umma.

"malalamiko" ni hali ya Mtumishi wa Umma kutoridhika na jambo alilotendewa au kutotendewa na Mwajiri, Mamlaka ya Ajira, Mamlaka ya Nidhamu au Mamlaka nyingine kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma.

"Mamlaka ya Ajira" maana yake ni mtu au chombo chochote chenye mamlaka ya kuajiri katika Ofisi ya Umma.

"Mamlaka ya Nidhamu" maana yake ni mtu au chombo kilichopewa mamlaka chini ya Katiba, Sheria ya Utumishi wa Umma au Sheria nyingine au mtu mwingine aliyekasimiwa mamlaka kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mtumishi wa Umma aliye chini yake.

“Mamlaka ya Rufaa” ni mtu au chombo kilichopewa Mamlaka na Sheria ya Utumishi wa Umma kuamua rufaa ya Mtumishi wa Umma au Mamlaka ya Nidhamu.

“Mwajiri” maana yake ni mtu au Taasisi katika Utumishi wa Umma ambayo Mtumishi wa Umma ameingia nayo mkataba wa ajira na ambayo ina wajibu wa kumlipa mshahara na stahili nyingine za kiutumishi kwa mujibu wa Sheria.

“Mtendaji Mkuu” maana yake ni Katibu Mkuu, Mkuu wa Idara Inayojitegemea, Katibu Tawala wa Mkoa, Mkurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Katibu wa Bunge, Naibu Katibu Mkuu, Mtendaji Mkuu wa Mahakama na wengine wanaotajwa na Sheria nyingine.

“Tume” maana yake ni Tume ya Utumishi wa Umma.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Mwongozo wa Mashauri ya Nidhamu, Rufaa na Malalamiko katika Utumishi wa Umma ni maelekezo mahsusi kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira, Mamlaka za Nidhamu, Mamlaka za Rufaa na Watumishi wa Umma kuhusu hatua wanazopaswa kuchukua kuhusu uendeshwaji wa mashauri ya nidhamu, rufaa na malalamiko kulingana na Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Nyaraka mbalimbali zinazosimamia Utumishi wa Umma. Mwongozo huu una Sura Nne. Sura ya Kwanza ni Utangulizi, Sura ya Pili ni Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa Umma, Sura ya Tatu ni Rufaa katika Utumishi wa Umma na Sura ya Nne ni kuhusu Malalamiko katika Utumishi wa Umma.

### 1.1 Madhumuni

Madhumuni ya Mwongozo huu ni kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa tafsiri na uelewa tofauti wa Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma hali inayoathiri misingi ya kushughulikia nidhamu, rufaa na malalamiko kwa haki, usawa na uwazi.

Mwongozo wa Mashauri ya Nidhamu, Rufaa na Malalamiko katika Utumishi wa Umma Toleo la Tatu umetokana na maboresho yaliyofanyika katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 na Kanuni zake. Mwongozo huu utawahusu watumishi wote wa Umma wakiwemo watumishi wa Taasisi za Umma na Wakala za Serikali wanaotawaliwa na Sheria zao ambao wanaelekezwa kuzingatia utaratibu uliotolewa katika Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2022 kwa ukamilifu kabla ya kuanza kushughulikia masuala ya nidhamu, rufaa na malalamiko kwa mujibu wa Sheria za Taasisi zao.

Hivyo, kufuatia marekebisho mbalimbali ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma yaliyofanyika mwaka 2022, Tume imelazimika kuhuisha Mwongozo wa Mashauri ya Nidhamu na Rufaa kwa Watumishi wa Umma Toleo la Pili la mwaka 2011 ili kuendana na wakati uliopo.

## 1.2 Watekelezaji wa Mwongozo

Utekelezaji wa masuala ya nidhamu ndani ya Utumishi waUmma ni jukumu la Mamlaka mbalimbali zilizopewa uwezo kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira katika Utumishi wa Umma, Sheria ya Utumishi wa Umma, Kanuni za Utumishi wa Umma, Taratibu za Uendeshaji wa Utumishi wa Umma pamoja na Taratibu Bora za Uendeshaji wa Mashauri ya Nidhamu katika Utumishi wa Umma. Hivyo, watekelezaji wa Mwongozo huu ni Waajiri, Mamlaka za Ajira, Mamlaka za Nidhamu, Mamlaka za Rufaa na Watumishi wa Umma ambao ni wanufaika wa maelekezo yaliyomo katika Mwongozo huu.

# SURA YA PILI

## 2.0 MAMLAKA ZA NIDHAMU KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Sura hii inaainisha Mamlaka za Nidhamu, aina ya makosa ya nidhamu na adhabu zake pamoja na taratibu za utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Nidhamu katika Utumishi wa Umma.

### 2.1 Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa Umma

#### (i) Rais

Kwa mujibu wa Kanuni ya 35(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022, Rais ni Mamlaka ya Nidhamu ya Katibu Mkuu Kiongozi.

#### (ii) Katibu Mkuu Kiongozi

Kwa mujibu wa Kifungu cha 4 (3) (d) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 kikisomwa kwa pamoja na Kanuni ya 35(2) (a) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, Katibu Mkuu Kiongozi ni Mamlaka ya Nidhamu kwa:-

- Makatibu Wakuu,
- Wakuu wa Idara Zinazojitegemea,
- Naibu Makatibu Wakuu,
- Makatibu Tawala wa Mikoa,
- Katibu wa Bunge,
- Mtendaji Mkuu wa Mahakama,
- Mkurugenzi wa Halmashauri za Serikali za Mitaa,
- Watumishi wengine watakaoteuliwa na Rais.

Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 4(4) chaSheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298, Katibu Mkuu Kiongozi ni Mamlaka ya Nidhamu ya juu kabisa katika Utumishi wa Umma. Kwa mujibu wa madaraka hayo, anaweza kumchukulia hatua ya kinidhamu mtumishi yeyote au kutekeleza Mamlaka yake aliyokasimisha kwa Mamlaka za Nidhamu.

**(iii) Waziri mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(a)(ii) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298, Waziri Mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaani Mamlaka ya Nidhamu ya Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa isipokuwa wanaoteuliwa na Rais.

**(iv) Makatibu Wakuu, Wakuu wa Idara Zinazojitegemea, Makatibu Tawala wa Mikoa na Mtendaji Mkuu wa Mahakama.**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(1)(b) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 na Kanuni ya 35(2)(b) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, Makatibu Wakuu, Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Wakuu wa Idara Zinazojitegemea na Makatibu Tawala wa Mikoa ni Mamlaka za Nidhamu kwa watumishi wote walio chini yao isipokuwa wale walioteuliwa na Rais.

**(v) Mamlaka ya Nidhamu kwa watumishi wa Wakala za Serikali na Taasisi za Umma**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 31(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298, Mamlaka ya Nidhamu kwa watumishi wa Umma walio katika Wakala za Serikali na Taasisi za Umma itakuwa kama ilivyoainishwa katika Sheria zilizoanzisha

Wakala na Taasisi hizo.

**(vi) Mamlaka ya Serikali za Mitaa**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(6) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298, Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni Mamlaka ya Nidhamu kwa watumishi wote wa Halmashauri isipokuwa wale walioteuliwa na Rais au Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa.

**(vii) Bodi ya Taasisi/ Mabaraza/ Tume**

Baadhi ya Sheria zilizoanzisha Taasisi zimezitaja Bodi za Taasisi/Mabaraza ya kitaaluma na Tume husika kuwa ni Mamlaka za Nidhamu.

## 2.2 Mamlaka nyingine za Nidhamu (Other Delegates)

Tume au Watumishi wa Umma waliokasimishwa mamlaka ya kutekeleza majukumu ya Rais chini ya Kifungu cha 21 cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298, watakuwa ni Mamlaka ya Nidhamu kwa watumishi wa Umma walioainishwa katika Kanuni zitakazotolewa na Rais wakati anakasimisha majukumu husika.

## 2.3 Makosa ya kinidhamu na adhabu zake

Kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, kuna aina mbili (2) za makosa ya nidhamu, ambazo ni:-

(a) Makosa mazito ambayo yameainishwa chini ya Kanuni ya 42(2), Jedwali la Kwanza, Sehemu A ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 na adhabu zake ni kufukuzwa kazi, kushushwa cheo na mshahara au kukatwa

mshahara ghafi kwa asilimia 15 kwa muda wa miaka mitatu (3) mfululizo.

Mtumishi wa Umma ambaye amepewa adhabu ya kushushwa cheo na mshahara atahesabika kuwa ameingia kwenye cheo kipya na atafikiriwa kupandishwa cheo muda wake utakapofika.

(b) Makosa mepesi ambayo yameainishwa chini ya Kanuni ya 43(1), Jedwali la Kwanza, Sehemu B, ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 na adhabu zake ni Onyo la Maandishi, Karipio kali na Kusitisha nyongeza ya mshahara.

Aidha, makosa mepesi yakifanywa na mtumishi kwa kujirudia zaidi ya mara nne ndani ya mwaka mmoja wa fedha, makosa hayo yanaingizwa kwenye makosa mazito.

(c) Ushughulikiaji wa makosa ya kinidhamu kwenye Wakala wa Serikali na Taasisi za Umma unaweza kutumia Sheria zake na pale zitakapokinzana na Sheria ya Utumishi wa Umma zitapaswa kuzingatia Sheria Kuu kwa jambo hilo kama ilivyoelekezwa katika Kifungu cha 34A cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 inayosomeka, kwa kunukuu;

***"Where there is any inconsistency between the provisions of this Act and any other law governing executive agencies, <u>public Intitutions or such other public service offices</u>, the provisions of this Act shall prevail".***

### 2.3.1 Utoaji wa Adhabu

Utoaji wa adhabu uzingatie uzito wa kosa na mambo mengine ambayo yanaongeza au kupunguza ukali wa kosa (mitigation factors). Adhabu itolewe pale tu kosa linapothibitika baada ya uchunguzi au mtumishi mtuhumiwa kukiri kosa moja kwa moja. Uamuzi wa Mamlaka ya Nidhamu utokane na makosa aliyoshtakiwa nayo mtumishi. Mamlaka ya Nidhamu baada ya kupokea Taarifa ya Uchunguzi itatafakari Taarifa hiyo na ushahidi uliowasilishwa na kutoa uamuzi wake ambapo itamjulisha mtumishi mtuhumiwa uamuzi huo ndani ya siku thelathini (30) tangu tarehe ya kupokea Taarifa ya Uchunguzi kwa mujibu wa Kanuni 48(6) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022.

### 2.3.2 Masuala ya Nidhamu na Makosa ya Jinai

Utaratibu wa kushughulikia mashauri ya nidhamu ambayo pia ni ya jinai umeelezwa chini ya Kanuni 50 (a -j), Kanuni 51(1) – (5) na Kanuni 52 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. Mtumishi anapokabiliwa na kesi ya Jinai mambo yafuatayo yatazingatiwa:-

i) Mtumishi hatafunguliwa mashtaka ya nidhamu mpaka kesi ya Jinai iishe Mahakamani.

ii) Mashtaka ya Nidhamu yakifunguliwa kisha mashtaka ya Jinai yakafunguliwa, mashtaka ya nidhamu yatasimama ‘’stayed’’ mpaka Mahakama itoe uamuzi.

iii) Mtumishi akiachiwa huru na Mahakama kwa sababu za kiufundi (on

legal technicalities), kuachiwa huko hakutakuwa kizuizi dhidi ya kufunguliwa upya mashtaka ya nidhamu na kuadhibiwa kana kwamba hakukuwa na Shauri la Jinai Mahakamani.

iv) Endapo atapatikana na hatia atahesabika kuwa ametiwa hatiani kwa makosa ya nidhamu kwa kuzingatia ushahidi ule ule uliotumiwa na mahakama. Kutokana na kutiwa hatiani, Mamlaka ya Nidhamu itamzuia kutekeleza majukumu yake (suspension) katika kipindi ambacho itakuwa inashughulikia hatma ya utumishi wake. Kabla ya kutoa uamuzi, Mamlaka ya Nidhamu inatakiwa impatie mtumishi Notisi ya kumtaarifu adhabu inayokusudiwa kutolewa ili mhusika aweze kutoa maelezo yake (mitigation) kuhusu kusudio hilo.

v) Shauri la jinai litahesabika kuwa limehitimishwa kama kutakuwa hakuna rufaa iliyokatwa au baada ya muda uliowekwa kisheria wa kukata rufaa kumalizika kwa mujibu wa Kanuni ya 51(1) - (2)] ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka, 2022.

vi) Endapo ataachiwa huru na Mahakama kwa sababu ya kutopatikana na hatia kwa makosa ya jinai aliyotuhumiwa nayo kutothibitika atastahili kurudishwa kazini mara moja na kulipwa stahiki zake zote za kiutumishi.

## 2.4 Majukumu na Maelekezo ya Utekelezaji

Mwongozo huu una Majedwali ya majukumu na maelezo ya utekelezaji pamoja na hatua zinazopaswa kuzingatiwa na Mamlaka ya Nidhamu katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama inavyooneshwa kwenye Jedwali la Kwanza. ***Kiambatisho "C".***

## SURA YA TATU

## 3.0 RUFAA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Sura hii inaainisha Mamlaka za Rufaa katika Utumishi wa Umma zilizopo kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 na utaratibu wa kukata rufaa endapo Mtumishi wa Umma au Mamlaka ya Nidhamu haikuridhika na uamuzi wa shauri la nidhamu au uamuzi wa Mamlaka ya rufaa uliotolewa na Mamlaka husika.

### 3.1 Mamlaka za Rufaa katika Utumishi wa Umma

Kwa mujibu wa Kifungu cha 25(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 kikisomwa pamoja na Kanuni ya 60(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, zifuatazo ni Mamlaka za Rufaa katika Utumishi wa Umma:-

**(i) Rais**

Rais ndiye Mamlaka ya Rufaa kwa watumishi ambao Mamlaka yao ya Nidhamu ni Katibu Mkuu Kiongozi. Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 25(1)(c) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298, mtumishi au Mamlaka ya Nidhamu ambayo haitaridhika na uamuzi uliotolewa na Tume ya Utumishi wa Umma anayo haki ya kukata rufaa kwa Rais ambaye uamuzi wake ni wa mwisho katika mkondo wa kiutawala.

**(ii) Tume ya Utumishi wa Umma**

(a) Kwa mujibu wa Kifungu cha 10(1) (d) na Kifungu cha 25(1)(b) vya Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 na kwa kuzingatia Kanuni ya 60(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, Tume ya

Utumishi wa Umma ni Mamlaka ya Rufaa kwa watumishi wote ambao Mamlaka zao za Nidhamu ni:

- Waziri Mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa,
- Katibu Mkuu,
- Mkuu wa Idara inayojitegemea,
- Katibu Tawala wa Mkoa,
- Mamlaka ya Serikali za Mitaa,
- Wakuu wa Idara na Divisheni, na
- Wakuu wa Taasisi.

(b) Kwa mujibu wa Kifungu cha 32A cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 [Marejeo ya Mwaka 2019] Mtumishi wa Umma, analazimika kwanza, kutumia mkondo wa Kisheria ulioainishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake kabla ya kutumia/kutafuta nafuu/haki za kisheria zilizopo katika Sheria za Kazi.

## 3.2 Taratibu za Utekelezaji wa Majukumu ya Mamlaka ya Rufaa

### 3.2.1 Utaratibu wa jumla wa kuzingatia

Utaratibu wa kushughulikia masuala ya rufaa kwa Watumishi wa Umma utazingatia mambo yafuatayo: -

(i) Kuthibitisha uwepo wa uamuzi unaopingwana Mrufani.

(ii) Kuhakiki muda uliotumika kuwasilisha rufaa.

### 3.2.2 Kuwasiliana na Mamlaka ya Nidhamu au Rufaa

Mamlaka ya Rufaa itawasiliana na Mamlaka ya Nidhamu ili kuomba majibu ya hoja na vielelezo vilivyotumika katika mchakato wa nidhamu unaopingwa na Mrufani. Mamlaka ya Nidhamu itatakiwa kuwasilisha majibu ya hoja na vielelezo ndani ya siku 14 tangu ilipopokea barua ya Mamlaka ya Rufaa.

### 3.2.3 Kumfahamisha Mrufani na Mamlaka ya Nidhamukuhusu uamuzi wa Rufaa.

Baada ya kukamilika kwa mchakato wa rufaa, Mrufani na Mrufaniwa (Mamlaka ya Nidhamu) watajulishwa uamuzi uliotolewa ikiwa ni pamoja na kujulishwa Mamlaka ya Rufaa inayofuata endapo Mrufani au Mrufaniwa hataridhika na uamuzi uliotolewa.

## 3.3 Majukumu na maelekezo ya utekelezaji

Mwongozo huu una Majedwali ya majukumu na maelezo ya utekelezaji pamoja na hatua zinazopaswa kuzingatiwa na Mamlaka ya Rufaa katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ilivyooneshwa katika Jedwali la Pili ***Kiambatisho "D"***

## SURA YA NNE

## 4.0 MALALAMIKO KATIKA UTUMISHI WA UMMA

Kwa mujibu wa Kifungu cha 10(1)(g) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 kikisomwa kwa pamoja na Kanuni 73(1)(b) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, Tume ya Utumishi wa Umma imepewa Mamlaka ya kushughulikia Malalamiko ya Watumishi wa Umma.

### 4.1 Utaratibu wa kuwasilisha malalamiko

Utaratibu wa Watumishi wa Umma kuwasilisha malalamiko utafuata ngazi zifuatazo:-

#### 4.1.1 Mwajiri

Malalamiko ya Mtumishi wa Umma dhidi ya Mkuu wa Idara katika Taasisi na Mashirika ya Umma yapelekwe kwa Mwajiri au Mkuu wa Taasisi.

#### 4.1.2 Bodi za Taasisi

Malalamiko ya mtumishi wa Umma dhidi ya Mwajiri au Mkuu wa Taasisi yapelekwe kwa Bodi ya Taasisi/Tume/Baraza la Uamuzi husika.

#### 4.1.3 Katibu Mkuu wa Wizara husika

Malalamiko ya Watumishi wa Umma wa Taasisi za Umma wasioridhika na uamuzi wa Mwajiri wao yapelekwe kwa Katibu Mkuu katika Wizara inayosimamia Taasisi au Shirika husika.

#### 4.1.4 Katibu Mkuu - UTUMISHI

Malalamiko ya watumishi wa Umma ambao hawakuridhika na uamuzi wa Mwajiri ama wa Katibu Mkuu wa Wizara husika yawasilishwe kwa Katibu Mkuu - UTUMISHI.

#### 4.1.5 Tume ya Utumishi wa Umma

Malalamiko ya Watumishi wa Umma waliopo Serikali Kuu, Idara Zinazojitemea, Wakala wa Serikali, Taasisi za Umma na Serikali za Mitaa ambao si wateuliwa wa Rais, yawasilishwe Tume ya Utumishi wa Umma endapo hawataridhika na Uamuzi wa Katibu Mkuu UTUMISHI.

#### 4.1.6 Katibu Mkuu Kiongozi

Malalamiko ya Watumishi wa Umma ambao hawajaridhishwa na uamuzi uliotolewa na Tume ya Utumishi wa Umma yapelekwe kwa Katibu Mkuu Kiongozi ambaye uamuzi wake utakuwa wa mwisho kiutawala. Vilevile, Watumishi wa Umma wanaoteuliwa na Rais walio na malalamiko watayawasilisha kwa Katibu Mkuu Kiongozi.

### 4.2 Mambo ya Kuzingatia katika Ushughulikiaji wa Mlalalamiko katika Utumishi wa Umma:-

#### 4.2.1 Muda wa kuwasilisha malalamiko

Malalamiko yapelekwe kwa Mamlaka husika ndani ya muda wa miezi kumi na mbili (12) tangu Mlalamikaji aliponyimwa haki au stahili anayolalamikia.

### 4.2.2 Uthibitisho wa malalamiko

Mlalamikaji ana jukumu la kuwasilisha ushahidi unaothibitisha malalamiko yake kwa Mamlaka husika.

### 4.2.3 Muda wa kushughulikia malalamiko

Mamlaka inatakiwa kushughulikia malalamiko ndani ya siku 90 na endapo Mamlaka itashindwa kushughulikia ndani ya muda huo, Mlalamikaji anaweza kuwasilisha malalamiko yake katika ngazi ya juu kama zilivyoainishwa katika Mwongozo huu.

### 4.2.4 Kuhitimishwa kwa Malalamiko na Utoaji wa Uamuzi

Maelekezo ya utekelezaji kuhusu masuala yanayopaswa kuzingatiwa na Mamlaka ya kushughulikia malalamiko yamebainishwa katika Miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Ajira, Mwongozo wa Mashauri ya Nidhamu, Rufaa na Malalamiko, Taratibu za Uendeshaji Bora wa Masuala ya Ajira na Taratibu za Uendeshaji Bora wa Masuala ya Nidhamu.

## 5.0 TANGAZO LA MGONGANO WA MASLAHI

Viongozi na watumishi wa Mamlaka zinazohusika katika kushughulikia Malalamiko na Rufaa za watumishi wa Umma katika mchakato mzima wa ushughulikiaji wa Malalamiko na Rufaa hizo, watatakiwa kutoa Tangazo la Mgongano wa maslahi kabla au wakati wa kushughulikia Malalamiko na Rufaa hizo ili haki si tu itendeke bali ionekane kutendeka. Pale ambapo mtumishi ametoa tangazo la mgongano wa maslahi, Mamlaka husika itabidi kuangalia mazingira husika na inapobidi mtoa Tangazo asihusike katika mchakato huo.

## 6.0 HITIMISHO

Kila Mwajiri, Mamlaka ya Ajira, Mamlaka ya Nidhamu, Mamlaka ya Rufaa pamoja na Watumishi wa Umma wanapaswa kuzingatia kikamilifu Mwongozo huu.

## 7.0 TAREHE YA KUANZA KUTUMIKA

Mwongozo wa Mashauri ya Nidhamu, Rufaa na Malalamiko katika Utumishi wa Umma Toleo Namba 3 la Mwaka 2024 utaanza kutumika mwezi Desemba, 2024 na unafuta Mwongozo kuhusu Mashauri ya Nidhamu na Rufaa kwa Watumishi wa Umma Toleo Namba 2 la Mwaka 2011.

## MFANO WA HATI YA MASHTAKA NA NOTISI

***Kiambatisho "A"***

**Notisi**

*(KANUNI YA 44(5)*

*Bw/Bi. ………… wa S. L. P……... Arusha, (Cheo). Ninakutaarifu kuwa ninakusudia kukufungulia mashtaka. Nakala ya Hati ya mashtaka imeambatishwa pamoja na taarifa hii.*

*Unatakiwa kutoa maelezo yako ya utetezi kwa maandishi kuhusu tuhuma iliyotajwa/zilizotajwa ndani ya Hati ya Mashtaka na unatakiwa kuwasilisha maelezo/utetezi huo katika muda wa siku kumi na nne (14) tangu tarehe ya kupokea taarifa hii.*

*Tambua kwamba, kama utetezi wako hautanifikia katika muda uliotajwa hapo juu, kwa kuzingatia Kanuni ya 45 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 nitaendelea na hatua za kukuchukulia hatua za kinidhamu bila kukupa taarifa tena.*

*Tarehe……………………….....* *..………………..………………*

*(Saini)*

*(Jina) Mamlaka ya Nidhamu*

***UTHIBITISHO***

*Mimi……………………………………………………………………..*
*Ninathibitisha kuwa nimepokea Hati ya Mashtaka na Notisi leo tarehe…………..……... mwezi……………….... mwaka 2024.*

***Kiambatisho “B”***

*HATI YA MASHTAKA*
*(Kanuni ya 44 (3))*

*SHTAKA*
*Kutokuwepo kazini kwa zaidi ya siku tano (5) bila ruhusa ya Mwajiri au sababu za msingi kinyume na Kanuni ya 42, Jedwali la Kwanza, Sehemu A, Aya ya 4 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022*

*MAELEZO YA SHTAKA*
*Bw./Bi……………………………..….. wa S. L. P..................Arusha, ukiwa mtumishi wa Umma katika Chuo cha Uhasibu Arusha kama Mkufunzi ulitenda kosa la kutokuwepo kazini bila ruhusa ya mwajiri wako kwa siku…… kuanzia tarehe …..…... hadi ….…....…*

*Tarehe………………...* *……………...……………….*
*(Saini)*
*(Jina) Mamlaka ya Nidhamu*

***Kiambatisho "C"***

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| 1. | **Kuanzisha hatuaza nidhamu.** | (i) Kufanya uchunguzi wa awali. | Kufanya uchunguzi wa awali ili kujiridhisha iwapo kuna ulazima wa kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya mtumishi. | Kanuni ya 36 ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | (ii) Kumpumzisha mtumishi kutekeleza majukukumu. | (i) Mamlaka ya Nidhamu kadri itakavyoona inafaa inaweza kuhusisha vyombo vingine vya uchunguzi kufanya uchunguzi. | Kanuni ya 37(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (ii) Iwapo kuna ulazima Mamlaka ya Nidhamu inaweza kumpumzisha kutekeleza majukumu yake bila kuathiri maslahi yake wakati uchunguzi wa awali unafanyika. | Kanuni ya 37(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (iii) Muda wa kumpumzisha mtumishi ni miezi mitatu (3) na pale ambapo kuna ulazima wa kuongeza muda kibali kiombwe kwa Katibu Mkuu (UTUMISHI). Iwapo KatibuMkuu (UTUMISHI) ni Mamlaka ya Nidhamu, kibali kiombwe kwa Katibu Mkuu Kiongozi. | Kanuni ya 37(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| | | | (iv) Muda wa nyongeza wa kumpumzisha mtumishi kutekeleza majukumu yake ni miezi miwili. | Kanuni ya 37(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (v) Mtumishi atapaswa kuendelea na majukumu yake endapo Mamlaka ya Nidhamu itashindwa kuzingatia muda wa kumpumzisha kazi. | Kanuni ya 37(4) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (vi) Endapo uchunguzi huo utahusisha vyombo vingine vya uchunguzi kutoka nje ya Ofisi, Mamlaka ya Nidhamu itaomba kibali kwa Katibu Mkuu Kiongozi na uchunguzi huo hautazidi kipindi cha miezi sita (6). | Kanuni ya 37(7) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022, Kanuni ya 37(7) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (vii) Mtumishi anayekabiliwa na tuhuma za kinidhamu asihamishwe mpaka shauri la nidhamu dhidi yake litakapohitimishwa. | Waraka wa Katibu Mkuu (UTUMISHI) wenye Kumb. Na.EA.45/257/01/18 wa tarehe21/05/2009. |

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| | | | (viii) Endapo itabainika kuwa mtumishi aliyehamishwa ana makosa ya kinidhamu aliyoyatenda kabla ya kuhamishwa kwake, mtumishi huyo atarejeshwa katika kituo chake cha awali kujibu tuhuma dhidi yake. | Waraka wa Katibu Mkuu (UTUMISHI) wenye Kumb.Na.EA.45/257/01/18 wa tarehe 21/05/2009. |
| | | | (ix) Hati ya mashtaka ieleze Kanuni iliyokiukwa na namna kosa lilivyotendeka. | Kanuni ya 44(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | Mamlaka ya Nidhamu inaweza kumsimamisha kazi mtumishi endapo:- | |
| | | | (i) itaona kuwa ni kwa manufaa ya Umma. | Kanuni ya 38(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (ii) atakuwa na kesi ya jinai Mahakamani. | Kanuni ya 38(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| 2. | **Kuamua mwenendo wa kufuata (Makosa Mepesi au Mazito)** | Mamlaka ya Nidhamu kumjulisha mtumishi mtuhumiwa hatua zinaoendelea dhidi yake. | Mamlaka ya Nidhamu kumpa mtumishi mtuhumiwa Notisi na Hati ya Mashtaka (na siyo barua) na kumtaka ajitetee. | Kanuni ya 44 (1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| | | | **Sifa ya Hati ya Mashtaka** | |
| | | | (i) Hati ya Mashtaka isainiwe na Mamlaka ya Nidhamu ya mtumishi husika. Aidha, kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, atakayesaini hati ya mashtaka ni Mkurugenzi. | Kanuni ya 44(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (ii) Hati ya Mashtaka ioneshe kwa ufasaha kosa na kifungu cha Sheria au Kanuni iliyokiukwa na mtumishi mtuhumiwa. Aidha, iainishe kwa ufasaha maelezo ya Shtaka ili kumwezesha mtumishi mtuhumiwa kuelewa tuhuma zinazomkabili ili aweze kujitetea ipasavyo. | Kanuni ya 44(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (iii) Hati ya Mashtaka iambatishwe na Notisi yenye maelezo ya kumtaka mtumishi mtuhumiwa kutoa utetezi wake katika muda wa siku 14 tangu tarehe ya kupokea Notisi na Hati ya mashitaka. | Kanuni ya 44(6) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| | | | (iv) Endapo mtumishi mtuhumiwa hajulikani alipo Notisi na Hati ya Mashtaka vipelekwe mahali alipokuwa anaishi au vitumwe kwenye anwani aliyokuwa anatumia mara ya mwisho. | Kanuni ya 57(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | **Mwenendo wa Makosa Mepesi** | Kanuni ya 43 (1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (i) Endapo mtumishi mtuhumiwa ana tuhuma za kufanya makosa mepesi, Mamlaka ya Nidhamu itaandaa na kumkabidhi Notisi na Hati ya Mashtaka. | Kanuni ya 49(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (ii) Hati ya Mashtaka itaonesha muda ambapo mtumishi mtuhumiwa atatakiwa kujitetea. | Kanuni ya 49(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (iii) Endapo Mamlaka ya Nidhamu itaona kuwa kuna haja ya kufanya uchunguzi, mtumishi mtuhumiwa atapewa haki ya kuitwa katika uchunguzi ili aweze kufanya utetezi wake dhidi ya tuhuma. | Kanuni ya 49(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| | | | Endapo mtumishi mtuhumiwa atashindwa kujitetea ndani ya kipindi alichopewa, Mamlaka ya Nidhamu itathibitisha tuhuma dhidi yake na kumpatia adhabu stahiki kama zilivyoorodhesha katikasehemu B ya Jedwali la Kwanza la Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. | Kanuni ya 49(4) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | **Mwenendo wa Makosa Mazito** Ushughulikiaji wa makosa mazito utazingatia mwenendo wa makosa mazito | Kanuni ya 42(1) na 44(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (i) Mamlaka ya Nidhamu itampa Hati ya Mashtaka na Notisi mtumishi mtuhumiwa (na siyo barua) na kumtaka ajitetee. | Kanuni ya 44(6) ya Kanuni za Utumishi wa Umma 2022. |
| | | | (ii) Mtumishi atasimamishwa kazi na Mamlaka ya Nidhamu baada ya kupewa Hati ya Mashtaka na Notisi. Mtumishi husika hataruhusiwa kutoka nje ya kituo chake cha kazi bila ruhusa ya Mamlaka ya Nidhamu. | Kanuni ya 38(1) na Kanuni ya 38(8) ya Kanuni za Utumishi wa Umma 2022. |

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| | | | (iii) Mtumishi aliyesimamishwa kazi ataendelea kupokea mshahara wake. | Kanuni ya 38(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma 2022. |
| | | | (iv) Mamlaka ya Nidhamu inaweza kumsimamisha kazi mtumishi endapo itaona kuwa ni kwa manufaa ya Umma. | Kanuni ya F.30(1) za Kanuni za Kudumukatika Utumishi wa Umma za mwaka 2009. |
| 3 | **Kuunda Kamati ya Uchunguzi** | Mamlaka ya Nidhamu kuunda Kamati ya Uchunguzi. | (i) Kuandika barua ya uteuzi wa Mwenyekiti na wajumbe wa Kamati ya Uchunguzi pamoja na kutoa hadidu za rejea kwa Kamati ya Uchunguzi. | Kanuni ya 45(1) na 46(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (ii) Kamati ya Uchunguzi kuanza kazi ndani ya siku 60 tangu mtumishi mtuhumiwa alipopewa Hati ya Mashtaka. | Kanuni ya 47(15) ya Kanuni za utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (iii) Mwenyekiti wa Kamati ya Uchunguzi ateuliwe kutoka nje ya Taasisi husika. | Kanuni ya 46(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (iv) Muundo wa Kamati uzingatie jinsi (sex), | Kanuni ya 46(5) ya Kanuni za utumishi wa Umma za mwaka 2022 |
| | | | (v) Wajumbe wa Kamati ya Uchunguzi lazima wawe na cheo cha Uandamizi na kuendelea. | Kanuni ya 46(1) (a) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| | | | (vi) Wajumbe wa Kamati wanaweza kuwa na cheo kinacholingana na cheo cha Mtumishi mtuhumiwa au zaidi. Iwapo Mamlaka ya Uteuzi wa mtuhumiwa ni Rais, Kamati ya Uchunguzi itaundwa na Jaji, Katibu Mkuu, Mkuu wa Idara inayojitegemea, Katibu Tawala wa Mkoa au Hakimu Mkazi Mwandamizi/ Hakimu Mkazi Mkuu. | Kanuni ya 46(1) (b) na 46(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (vii) Kamati iwe na wajumbe wasiopungua wawili (2) na wasiozidi wanne (4). | Kanuni ya 46(4) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (viii) Iwapo Kamati itahitaji utaalam maalum, itaomba kwa Mamlaka ya Nidhamu ambayo itawajibika kuwapata wataalam husika. | Kanuni ya 46(6) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (ix) Kamati ya Uchunguzi ifanye kazi ndani ya siku 60. Iwapo itahitaji muda wa nyongeza itaiomba Mamlaka ya Nidhamu ambayo itaongeza muda usiozidi siku 30. Ikiwa uchunguzi hautakamilika ndani ya muda ulioongezwa, Mamlaka ya Nidhamu itaomba idhini Mamlaka ya Nidhamu itaomba idhini | Kanuni ya 47(17) na 47(18) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| | | | ≈ Mkuu - UTUMISHI ya kuongeza mudawa kuendelea na uchunguzi. | |
| 4 | **Kuchunguza tuhuma** | Kamati ya Uchunguzi kupitia tuhuma na utetezi. | (i) Kamati ya Uchunguzi kumfahamisha Mtuhumiwa siku, tarehe, muda na mahali pa kufanyia kikao cha Uchunguzi siku 7 kabla ya tarehe ya kikao. | Kanuni ya 47(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (ii) Barua ya wito ipelekwe mahali ambapo mtumishi husika anaishi, kufanya kazi au anwani yake ya mwisho. | Kanuni ya 47(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (iii) Mtumishi mtuhumiwa akikataa kufika mbele ya Kamati ya Uchunguzi bila sababu za msingi atachukuliwa hatua za kinidhamu. | Kanuni ya 47(4) za Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (iv) Mtuhumiwa na Mamlaka ya Nidhamu wajulishwe na kupewa haki zote za kisheria wakati wa uchunguzi. | Kanuni ya 47(5), 47(7) na 47(9) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (v) Uchunguzi uanze kufanyikandani ya muda wa siku sitini (60) tangu siku ambayo | Kanuni ya 47(15) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| | | | mtumishi mtuhumiwa alipewa hati ya mashitaka. | |
| | | | (vi) Ikiwa wakati uchunguzi ukiendelea itabainika tuhuma mpya, Mamlaka ya Nidhamu itajulishwa na itampa mtuhumiwa hati ya mashtaka kwa tuhuma hizo mpya kabla hazijachunguzwa. | Kanuni ya 47(13) na 47 (14) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (vii) Taarifa izingatie Hadidu za rejea na iandaliwe kwa kuzingatia nyongeza Na. 3. | Maelekezo Mahsusi kwa Mamlaka za Nidhamu na Kamati za Uchunguzi kuhusu namna ya kuendesha uchunguzi wa mashauri ya Nidhamu Na. 1 ya mwaka 2008. |
| | | | (viii) Kamati ya Uchunguzi kumpa Mwenendo wa Uchunguzi Mtumishi mtuhumiwa ili apitie na kutoa maoni yake iwapo yaliyoandikwa ndiyo yaliyozungumzwa na asaini kila kurasa ya Mwenendo. | Aya ya 25.3.3 (c) ya Taratibu Bora za Uendeshaji wa Masuala ya Nidhamu za mwaka 2007. |

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| | | | (ix) Mamlaka ya Nidhamu kumpa Mtumishi Mwenendo wa Kamati ya Uchuguzi iwapo ataomba baada ya Uchunguzi kukamilika. | Kanuni ya 48(7) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| 5 | **Kuhitimishwa kwa Uchunguzi** | Kamati ya Uchunguzi kuwasilisha Mwenendo wa Uchunguzi na Ripoti ya Uchunguzi kwa Mamlaka ya Nidhamu. | (i) Taarifa ya Uchunguzi ieleze wazi endapo tuhuma dhidi ya mtumishi zimethibitishwa au vinginevyo pamoja na vigezo vilivyotumika kuthibitisha,maoni ya Kamati ya Uchunguzi kuhusu mambo yaliyochangia katika kuongeza au kupunguza uzito wa tuhuma na mambo mengine muhimu. | Kanuni ya 48(2) (a) -(c) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (ii) Taarifa ya Kamati iwe na mapendekezo kuhusu aina ya adhabu itakayotolewa kwa mujibu wa Sheria. | Kanuni ya 48(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (iii) Baada ya Mamlaka ya Nidhamu kupitia Taarifa ya Uchunguzi, endapo itabaini kuwa uchunguzi zaidi unahitajika, itarejesha Taarifa hiyo kwa Kamati ya Uchunguzi Pamoja na maelekezo kadri itakavyoona inafaa. | Kanuni ya 48(4) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| | | | (iv) Kamati ya Uchunguzi itafungua tena uchunguzi kufuatia maelekezo ya Mamlaka ya Nidhamu kwa mujibu wa kanuni ya 47. | Kanuni ya 48(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| 6. | **Hitimisho la Shauri la Nidhamu** | Mamlaka ya Nidhamu Kutafakari na kutoa adhabu | (i) Baada ya kupokea Taarifa ya Uchunguzi na kutafakariushahidi na taarifa hiyo Mamlaka ya Nidhamu itatoa uamuzi na kumjulisha mtumishi mtuhumiwa kuhusu uamuzi huo katika muda wa siku thelathini (30) kuanzia tarehe ya kupokea taarifa ya Kamati ya Uchunguzi. | □ Kanuni ya 48(6) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (iii) Kushindwa kutoa uamuzi ndani ya siku 30 kutatafsiriwa kuwa mtumishi mtuhumiwa hana hatia. | Kanuni ya 48(11) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (iv) Mtumishi aelezwe haki, mahalina muda wa kukata rufaa. | Kanuni ya 60 na 61 ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| 7. | **Mtumishi anayekabiliwa na Kesi ya jinai Mahakamani** | Mamlaka ya Nidhamu kufanya tathmini ili kubaini endapo kosa | (i) Shauri la Nidhamu halitafunguliwa endapo mtumishi anakabiliwa na kesi ya jinai Mahakamani. | Kanuni ya 50(a) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| | | analotuhumiwa mtumishi pia ni kosa la jinai. | (ii) Mtuhumiwa anaweza kusimamishwa kazi hadi shauri la jinai litakapomalizika. | Kanuni ya 38(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka, 2022. |
| | | | (iii) Endapo shauri la nidhamu litakuwa limeanzishwa na kesi ya jinai ikafunguliwa mahakamani shauri la nidhamu litasimama kupisha kuhitimishwa kwa kesi ya jina. | Kanuni ya 50(b), ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (iv) Endapo mtumishi atatiwa hatiani kwa makosa ya jinai itachukuliwa kuwa makosa ya nidhamu yamethibitika na Mamlaka ya Nidhamu itaendelea kutoa adhabu bila kuanzisha au kuendelea na shauri la kinidhamu dhidi yake. | Kanuni ya 50(e) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |
| | | | (v) Kama Mtumishi atatiwa hatiani kwa makosa ya jinai itakuwa ni ushahidi wa kuthibitisha kuwa Mtumishi husika alitenda makosa ya nidhamu kwa kuzingatia mazingira ya makosa ya jinai aliyotiwa hatiani. | Kanuni ya 50(i) ya Kanuni za Utumishi wa Umma, 2022. |

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| | | | (vi) Endapo Mtumishi atakuwa ametiwa hatiani na Mahakama, Mamlaka ya Nidhamu inapaswa kusubiri hadi muda wa kukata Rufaa Mahakamani utakapokwisha na kujiridhisha iwapo Mtumishi alikata rufaa au la. | Kanuni ya 51(a)(b) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (vii) Endapo Mtumishi atakuwa amekata rufaa Mahakamani, Mamlaka ya Nidhamu inapaswa kusubiri uamuzi wa Mahakama. | Kanuni ya 51 (b) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (viii) Mtumishi wa Umma akiachiwa Mahakamani kwa sababu za kiufundi haitazuia Mamlaka ya Nidhamu kumchukulia hatua za kinidhamu. | Kanuni ya 50 (c) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (ix) Endapo ataachiwa huru na Mahakama kwa sababu ya kutopatikana na hatia kwa makosa ya jinai aliyotuhumiwa nayo kutothibitika atastahili kurudishwa kazini mara moja na kulipwa stahiki zake zote za kiutumishi. | |

| JEDWALI I: MAJUKUMU YA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MASHAURI YA NIDHAMU | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NA.** | **JUKUMU** | **KAZI** | **KWA MAMLAKA ZA NIDHAMU** | **REJEA** |
| | | | (x) Shufaa/Maombelezo (Mitigation) Mamlaka ya Nidhamu na Rufaa zinatakiwa kuzingatia historia ya mtuhumiwa utendaji kazi wake wa siku za nyuma na tabia ya mtuhumiwa ili zisaidie mamlaka ya Nidhamu kupunguza adhabu. | Kanuni ya 48(1) (b) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2022. |

*Kiambatisho "D"*

**JEDWALI II:MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI KWA MAMLAKA ZA RUFAA**

| Na. | JUKUMU | KAZI | HATUA ZA UTEKELEZAJI NA MAMBO YA KUZINGATIA | REJEA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Kupokea Rufaa** | Mamlaka ya rufaa kupokea rufaa. | (i) Kupokea rufaa. | Kanuni ya 60 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022 na Aya ya 25 ya Taratibu Bora za Uendeshaji wa Masuala ya Nidhamu za mwaka 2007. |
| | | | (ii) Kupitia vielelezo vya ushahidi vilivyowasilishwa na Mrufani (Barua ya Uamuzi wa shauri la nidhamu, Hati ya mashitaka na notisi na Utetezi wake) na kumtaarifu Mrufani endapo kuna upungufu wa baadhi ya vielelezo. | Aya ya 25.1.4 ya Taratibu Bora za Uendeshaji wa Masuala ya Nidhamu za mwaka 2007. |
| | | Kuwasiliana na Mamlaka ya Nidhamu/Rufaa | (i) Mamlaka ya Nidhamu iwasilishe majibu ya hoja za rufaa na vielelezo vya ushahidi vilivyotumika katika rufaa husika ndani ya siku 14 kuanzia tarehe kupokea maelekezo hayo. | Kanuni ya 61(3)(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (ii) Mamlaka ya Rufaa itaendelea kusikiliza rufaa endapo Mamlaka ya Nidhamu itashindwa kuwasilisha vielelezo kwa wakati bila kuwa na sababu za msingi. | Kanuni ya 61(4) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |

*Kiambatisho "D"*

**JEDWALI II:MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI KWA MAMLAKA ZA RUFAA**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2 | **Kutoa Uamuzi wa rufaa.** | Mamlaka ya Rufaa kutoa uamuzi. | (i) Mamlaka ya Rufaa kutoa uamuzi wa rufaa na kumtaarifu Mrufani na Mamlaka ya Nidhamu juu ya uamuzi huo. | Kanuni ya 60 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (ii) Mrufani na Mrufaniwa wajulishwe haki na mahali pa kukata rufaa wasiporidhika na uamuzi wa Tume. Endapo Mamlaka ya Rufaani Rais, uamuzi wake ni wa mwisho. | Kanuni ya 60(4) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |
| | | | (iii) Mrufani au Mrufaniwa wajulishwe muda wa kukata rufaa (ndani ya siku 45) tangu kupokea barua ya Uamuzi. | Kanuni ya 61(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2022. |

*Kiambatisho "E"*

**JEDWALI III:MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI KWA MAMLAKA YA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO**

| Na. | JUKUMU | KAZI | HATUA ZA UTEKELEZAJI NA MAMBO YA KUZINGATIA | REJEA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Kupokea Malalamiko** | Kupokea malalamiko. | (i) Kupokea na kushughulikia malalamiko kwa kusajili na kumjulisha Mlalamikaji kuhusu kupokelewa kwa malalamiko yake | |
| | | | (ii) Mamlaka kuwasiliana na Mwajiri/Mamlaka ya Ajira ya Mlalamikaji kumtaka kuwasilisha maelezo na vielelezo kuhusu malalamiko ya mtumishi husika ndani ya siku kumi nne (14) tangu kupokelewa kwa barua ya Tume. | |
| 2 | **Kuchambua na kutoa uamuzi wa malalamiko** | Kufanya uchambuzi. | (i) Kuchambua malalamiko kwa kuzingatia hoja na vielelezo vya ushahiidi vilivyowasilishwa na wahusika. | |
| | | | (ii) Uamuzi utatolewa na wahusika wajulishwe kuhusu uamuzi uliofikiwa na haki ya kuwasilisha malalamiko yao ngazi ya juu kama ilivyoainishwa na Mwongozo huu. | |
| | | | (iii) Kutunza kumbukumbu za uchambuzi wa malalamiko na kuziwasilisha kwenye Mamlaka endapo zitahitajika. | |

*Kiambatisho "E"*

**JEDWALI III:MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI KWA MAMLAKA YA KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO**

| Na. | JUKUMU | KAZI | HATUA ZA UTEKELEZAJI NA MAMBO YA KUZINGATIA | REJEA |
|---|---|---|---|---|
| | **Uamuzi wa Tume unaokatiwa Rufaa kwa Rais** | Jukumu la Tume | Kuwasilisha maelezo na vielelezo vinavyohusika kwa Rais iwapo ni Rufaa na kwa Katibu Mkuu Kiongozi iwapo ni malalamiko | |